# Uchanganuzi wa Matukio ya Uhalisiamazingaombwe katika Utendi wa Mikidadi na Mayasa: Kupigana kwa Mikidadi

***Emmilly Kemuma Onyancha, Sheila Pamela Wandera-Simwa, James Ogola Onyango***
**Chuo Kikuu Cha Laikipia, Kenya**

## Abstract

*This paper makes a critical analysis of how themes that mirror magic realism are presented in Utendi wa Mikidadi na Mayasa. The paper specifically focuses on tenets of magic realism that revolve around a character called Mikidadi. This epic poem was purposively sampled because it reflects the pillars of Magic Realism theory, that was founded by Franz Roh, in a remarkable way. Mikidadi is beyond the borders of an ordinary human being. He is engaged in many battles in which he vanquishes all his opponents save only in one battle with Ali (the Lion of God). This is indeed an affirmation of magic realism. It is expected that this paper will be useful to scholars of Kiswahili classical poetry and magical realism.*

**Key words:** Fighting, hero, killing, magic realism, robbing.

## Ikisiri

*Makala hii inachunguza mtindo wa kutumia matukio ya uhalisiamazingaombwe katika kuendeleza maudhui katika Utendi wa Mikidadi na Mayasa ulioandikwa na Elbuhry (1932). Makala hii imechunguza matukio ya uhalisamazingaombwe katika kiwango cha wahusika na hususan mhusika Mikidadi. Uteuzi wa utendi huu ulifanywa kimaksudi kwa sababu utendi umesheheni matukio ya uhalisiamazingaombwe. Shughuli hii iliongozwa na mihimili ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe iliyoasisiwa na Franz Roh. Mhusika Mikidadi amepewa nguvu ambazo si za kawaida. Nguvu za kupigana na kuwaua watu wengi ni jambo ambalo linachochea uamuzi kuwa huu si uhalisia bali ni uhalisiamazingaombwe. Katika vita vyote alivyohusika, Mikidadi amepigana kwa namna ambayo si ya kawaida na ameweza kuwapiku wapinzani wake wote isipokuwa Ali, Simba wa Mungu. Makala hii itawafaa wasomi watakaofanya tafiti zao katika kitengo cha mashairi ya jadi kwa kuwaongezea maarifa kuhusu nadharia hii ya uhalisiamazingaombwe.*

**Maneno Muhimu:** Kupigana, kuiba, kuua, shujaa, uhalisiamazingaombwe.

## Utangulizi

Makala hii imegawanywa katika sehemu tano kuu. Waandishi anaanza kwa kutoa muhtasari wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ili kumuweka msomaji katika hali ya uelewa wa yale yatakayojadiliwa katika makala nzima. Wanafuatiliza kwa kuelezea Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe kwa ufupi, na kufafanua mihimili yake iliyotumika katika kutambulisha matukio ya kihalisiamazingaombwe. Sehemu ya tatu ndiyo kiini cha makala hii ambapo waandishi wanachanganua matukio ya kihalisiamazingaombwe kwa kutumia mihimili teule ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Sehemu ya nne inatoa matokeo ya uchanganuzi kwa jumla, na kisha waandishi wanahitimisha makala kwa kuangazia madhumuni muhimu ya makala.

## Muhtasari wa Utendi wa Mikidadi na Mayasa

Utendi huu unahusu wahusika wawili wakuu yaani Mikidadi na Mayasa. Mayasa anapofika umri wa kuolewa anamwambia babake kuwa angekubali tu kuolewa na mwanamume ambaye yeye angepigana naye na kumshinda vitani. Wanaume wengi wanajitokeza kumtaka Mayasa mkono wa ndoa. Wanakuja wanaume wengi sana, ambao wengine anapigana nao na anawashinda na hatimaye anawaua, ilhali wengine wanaamua kuondoka bila kupigana naye. Katika pilka pilka hizo, panatokea mvulana kwa jina Mikidadi. Kama desturi, Mayasa anapigana na Mikidadi, na anaposhindwa kivita, Mayasa anakubali kuolewa naye. Mikidadi ndiye mwanamume pekee aliyeweza kulingana naye kinguvu, na basi kuwapiku wale wengine. Babake Mayasa anapinga ndoa hii kwa sababu Mikidadi hana mali. Jabir, baba yake Mayasa, anaamua kuomba mahari ya thamani kubwa akijua Mikidadi atashindwa kulipa, ili amuoze Mayasa kwa mwanamume ambaye ana mali. Mikidadi anaamua kuondoka kwenda kutafuta mali aliyoitishwa, na anapopata anarudi kumpa babamtu ili amruhusu amuoe bintiye Mayasa. Anapofika kwa mzee Jabir, anapata Mayasa ameshaozwa kwa Malik. Kwa bahati nzuri, akiwa njiani anakutana na jeshi ambalo lilikuwa likimpeleka Mayasa kwa Malik. Mikidadi anapigana na jeshi hili na kulizidi nguvu, na mwishowe anampata Mayasa. Jabir hakufurahishwa na jambo hili na basi anapanga njama ya kumuua Mikidadi ili kumrudisha Mayasa kwa Malik. Jabir anafanikiwa kumrudisha Mayasa kwa Malik, lakini Mikidadi anazidi kumwandama Malik, na mwishowe anamuua. Jabir pia anauawa kwa kukataa kuokoka. Baadaye, Mikidadi na Mayasa wanaamua kwenda mbinguni kupigana vita vitakatifu. Mikidadi na Mayasa wanapofika kwa mtume wanakaribishwa kwa kuandaliwa sherehe kubwa ambayo chakula chake kinamshibisha kila mmoja katika eneo hilo na jirani.

## Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe

Nadharia ya uhalisiamazingaombwe iliasisiwa na Franz Roh mwaka wa (1925). Nadharia hii hushughulikia matukio ambayo yamepita mipaka ya uhalisia hadi yakawa hayawezi kuaminika tena katika hali ya kawaida. Nadharia hii inahusishwa na waandishi wa Marekani ya kusini na nchi za ulimwengu wa kati. Walibora (2010), anasema kuwa uhalisiamazingaombwe katika *Dunia Yao* na *The Tin Drum* umetumia sifa bainifu za uhalisiamazingaombwe kama nyenzo za kuakisi na kuyumbayumba na ukosefu wa uthabiti na udumifu katika maisha Afrika na Ulaya. Uhalisiamazingaombwe hufafanua tofauti ambazo huyaelezea matukio ya kifantasia, kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida. Alexander (1990) anasema kwamba uhalisiajabu ni kielelezo cha jinsi nadharia ya usasa-leo inavyotulazimu kufikiria upya juu ya dhana ya kimapokeo kuhusu riwaya ya uhalisia ya karne za kumi na nane na tisa.

Kulingana na Zamora (1993 na 1995), Danow (1995), Cooper (1998) na Encarta encyclopaedia (2000), nadharia hii ina mihimili minane ambayo ni pamoja na: matukio ya kiajabu yanayoonekana ya kawaida, kuchanganyika kwa uhalisia na ndoto, kuvunjwa kwa mipaka ya kimataifa, kijamii na kitaifa, mambo kujirudia mahali kwingine, kutofuatana kwa matukio kimantiki kama ilivyo kawaida, kurejelewa kwa wanyama, misitu mikubwa, majitu, wanyama hatari na mazimwi, katika uandishi huu mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu na kuingiliana kwa hali mbalimbali kama vile uhalisi, kifo na uhai. Kati ya mihimili hiyo minane, makala hii iliteua mihimili miwili pekee, ambayo iliwezesha kutambulisha matukio ya uhalisiamazingaombwe katika muktadha wa vita vya Mikidadi. Mhimili wa kwanza uliotumika ni ule unaosema kuwa matukio ya kihalisiamazingaombe ni yale yanayoonekana ya kawaida lakini yanaogofya. Mhimili huu ulitumika kutambulisha kupigana kwa Mikidadi ambako kulionekana kama kupigana kwa kawaida, lakini kwa namna nyingine,

kwa jinsi alivyoua watu, kupigana huko kuliogofya kwa kiasi kikubwa na basi kutosheleza kuwekwa katika mkumbo wa uhalisiamazingaombwe.

Mhimili wa pili uliotumika ni ule unaodai kuwa matukio ya kihalisiamazingaombwe huvunja mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa. Mhimili huu ulitumika kutambulisha matukio ya kiajabu katika kupigana kwa Mikidadi, ambayo yaliweza kutanda kote licha ya mipaka ya kijamii na kitaifa. Mikidadi anapigana na watu wa karibu kama Malik. Pia, anapigana na watu wa matabaka tofauti tofauti na hivyo kuvunja mipaka ya kijamii. Katika nyanja za kitaifa na kimataifa, Mikidadi anavunja mipaka hii kwa kupigana na masultani mbalimbali pamoja na Ali, Simba wa Mungu.

## Matukio ya Uhalisiamazingaombwe

### *Kupigana kwa Mikidadi na Mayasa*

Mikidadi alikuwa maskini ambaye hata mahari ya kumlipia mke hakuwa nayo. Anaposikia kuwa Mayasa alikuwa anaozwa kwa mwanamume ambaye alihitajika apigane naye na amshinde vitani, anaamua kujitosa katika kinyang'anyiro hicho, licha ya kufahamu kuwa hana uwezo wa kifedha. Ijapokuwa Mikidadi alikuwa mtu wa kawaida tu, anapojitokeza kupigana na Mayasa, anaonyesha upekee ambao wale wanaume wengine hawakuwa nao, na ndio maana Mayasa anahiari kuolewa naye. Namna ya kupigana kwake inadhihirisha sifa walizokosa wanaume wenzake waliomtangulia. Jinsi anavyowaua watu wengi bila silaha, kabla ya kuanza kupigana na Mayasa ni tukio la ajabu. Katika ubeti wa 87, inaonyeshwa jinsi watu walivyomstaajabia Mikidadi:

*Wote walipomuona*
*Wakastaajabu sana*
*Yule ambaye awana*
*Na silaha akitwaa*

Kwa hivyo, tukio la kuwaangamiza watu wengi waliokuwa wamejiandaa na kubeba silaha za vita ni la kiajabu na basi linampendekeza kwa Mayasa anayekubali kuolewa naye dhidi ya wale wengine wote waliojiweza kihali na kimali. Mayasa anasema haya katika ubeti wa 121:

*Nakasa kamba babangu*
*Hata pasiwe na fungu*
*Huyu ndiye mume wangu*
*Shuruti imetimia*

Mifano hii miwili ya kupigana kwa Mikidadi na mingine itakayozungumziwa katika sehemu ifuatayo ndiyo usuli wa makala hii. Kupigana kwa Mikidadi na watu mbalimbali katika miktadha tofauti tofauti kunadhihirisha matukio ya uhalisiamazingaombwe katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na pia kuafiki mihimili miwili teule ya Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe.

### *Kupigana kwa Mikidadi na Jini*

Nyambung'a (2005) anasema kuwa matukio ya uhalisiamazingaombwe husawiriwa yakiwa ya kiajabuajabu, na ya kutisha. Tukio la Mikidadi kupigana na jini linaogofya kwa vile majini hayo hayaonekani! Kuamua kupigana na kiumbe ambaye humuoni, naye anakuona, ni jambo la kiajabu. Mikidadi anapofika, anaambiwa na jini arudi, naye analijibu jini kuwa lingalimfahamu, lisingalimwambia maneno hayo. Haya yanapatikana katika beti za177 na 178.

Zinaeleza hivi:

*Afriti karadidi*
*kamwambia Mikidadi*
*rejea kwenu urudi*
*waama utapotea*
*Mikidadi akanena*
*ewe jini maleuma*
*kama wanijua sana*
*hayo usengeniambia*

Jini linapojaribu kumuua Mikidadi, Mikidadi anaomba dua ya siri na jini hilo linakwenda zake likilalama kuwa linachomwa na moto. Mikidadi analishinda jini kivita mpaka jini linatoroka na kuacha maji lililokuwa likichunga. Hili ni tukio la kihalisiamazingaombwe kwa sababu halina uhalisia ndani yake, na si tukio la kawaida.

***Kupigana kwa Mikidadi na Sultani***

Wamitila (2008), ameliangazia swala la uhalisiamazingaombwe katika riwaya ambapo anaelezea jinsi uhalisiajabu huingiza sifa zinazofahamika na msomaji. Waandishi wa kazi za fasihi wanakubaliana na maoni ya Wamitila kuwa sifa zenyewe hufahamika na msomaji. Kwa mfano: Sultani alimfungia mvulana mmoja ambaye alinuia kumuua keshoye kusudi amchukue bibi yake Anasa. Mikidadi anamfungulia Kesa pamoja na wenzake aliokuwa nao, na kuwaweka juu ya jabali. Anamuuliza Kesa anachotaka afanyiwe. Luhani naye anamwambia amuue. Mikidadi anapigana na askari na kuwaua hamsini, Sultani anakasirika sana na kuamua kupigana na Mikidadi lakini mwisho anauawa na kichwa chake kinapelekewa Kesa. Haya yanajitokeza katika beti za 236 na 238:

*Akamshika Luhani*
*Kamwangusha farasini*
*Kamkalia kitwani*
*Na kisu kamshikia*

*Akamkata na tasu*
*Kwa mkonowe na kisu*
*Akamuekea kisu*
*Mbeleye kamuekea*

Kupigana kwa Mikidadi si kwa kawaida kwa sababu anapigana na watu wengi mno bila mpango wa awali. Anawaua wote, pamoja na kiongozi wao. Anavunja mipaka ya kijamii. Kwa mja asiye na mbele wala nyuma, kupigana na Sultani na jeshi lake na kuweza kuwashinda na kuwaua ni tukio la kihalisiamazingaombwe.

***Kupigana kwa Mikidadi na Askari Wengi***

Njogu na Chimera (2006) wanasema fasihi simulizi huzungumzia maajabu au mazingaombwe mengi ambayo katika hali halisi huwa hayawezi kutokea. Baadhi ya maajabu hayo huwa ni mashujaa ambao huwa na sifa ambazo hazibainiki kwa mtu wa kawaida. Mikidadi anapopatana na jeshi lingine anapigana nalo na kuua watu hamsini na kuchukua mali yao. Habari hizi zinamfikia Kasiri; kuwa kuna mwanamume aliye na nguvu kama simba, na ambaye

amesababisha njia kutopitika kwa sababu anapigana na wapita njia, na kutwaa mali yao. Kasiri alikasirika sana kwa sababu haelewi jinsi mtu wa kawaida mmoja anavyoweza kuwashinda askari wengi kiasi cha wao kuamua kutoroka. Kasiri basi anaamua kuwatuma askari mia tano wakamuue Mikidadi, lakini anapigana nao na kuwauwa askari mia moja, na waliobaki wakakimbia ili kuokoa maisha yao. Walipofika, walimueleza Kasiri yaliyojiri naye alikasirika sana. Alikasirishwa na hali kuwa mtu mmoja aliweza kuwaangamiza watu wengi hivyo, wakiwemo askari. Kasiri tena anawatuma askari wengine ambao walienda kwa baragumu na panda naye Mikidadi alipowaona aliwaendea na kupigana nao. Mikidadi aliwaua tena askari wengi, na waliosalia wakakimbia na kumwambia Kasiri asitume askari wengine tena. Kasiri haamini anayoambiwa kwa vile katika hali ya kawaida haya hayawezekani. Kasiri alighairi, na badala yake akatuma askari mashujaa elfu moja ambao pia waliangamizwa. Haya yote yanaelezewa katika beti za 286 hadi 300. Beti za 286, 299 na 300 zinasema hivi:

*Askari kawatenga*
*Wema wakushika panga*
*Hao waliojifunga*
*Ni watu khamsu mia*

*Wakangia kupigana*
*Kwa panga wakitemana*
*Muda punde kiwaona*
*Wafeleo watu mia*

*Wabaki wasalieo*
*Jamii wakenda mbio*
*Hata wakipata kwao*
*Sultani kamwambia.*

Kupigana huku ni tukio la kiajabu kwa sababu aghalabu mtu wa kawaida hawezi kuwaua watu wengi hivyo, hasa ikiwa watu hao ni askari wa taifa.

***Kupigana kwa Mikidadi na Sultani na Askari Wake***

Sultani alimtumia Mikidadi askari wamwangamize. Walipofika kwa Mikidadi walianza vita mara moja na baada ya muda mfupi Mikidadi alikuwa amewaua mamia wa askari hao. Mashujaa hao walirudi kwa Sultani kumuuliza walichostahili kufanya. Sultani aliwarejesha askari hao vitani, ambao safari hii walikuwa wameapa kupigana kwa uwezo wao wote. Siku hiyo, Mikidadi pia alijizatiti sana na akaua askari mia nne, na waliosalia wote wakakimbia. Haya yanaelezewa katika ubeti wa 329. Ubeti huo nasema hivi:

*Aloua siku hiyo*
*Mashujaa wanenayo*
*Hisabu niliyonayo*
*Shujaa aruba mia*

Huu ni uhalisia ambao umekiuka mipaka hadi ukawa hauaminiki (Rogers, 2002). Sultani aliamua kupigana na Mikidadi mwenyewe. Mikidadi alipomshinda Sultani, alimfanya mfungwa (ubeti 335). Shairi linasema:

*Akamfunga na pingu*
*Kwa ghadhabu na matungu*
*Akamba wataka langu*
*Kwenu kumekukataa*

Uwezo wa Mikidadi kupigana na kuwashinda askari mia nne ambao walikuwa wamejitolea kupigana kwa uwezo wao wote ni tukio la kiajabu kwani hawa si watu wa kawaida tu, bali ni mashujaa; ni askari. Na si askari tu, bali ni askari ambao walikuwa wamejitolea kupigana kwa uwezo na ustadi wao wote. Mikidadi pia anavunja mipaka ya kijamii kupitia vita vyake na Sultani, kwani yeye ni mtu wa tabaka la chini aisyestahili kutangamana na Sultani kwa vyovyote vile.

***Kupigana kwa Mikidadi na Sultani wa Kasri***

Sultani wa Kasri alisikia habari za ushujaa wa Mikidadi akamwamrisha waziri wake amlete Mikidadi kwake. Mikidadi alipofika kwa Sultani, mkuu huyo alimpa dinari elfu kumi na akamtaka apigane na askari mashujaa elfu moja. Sultani alikuwa ashuhudie vita hivyo. Beti za 369, 376 na 379 zinadhihirisha haya:

*Alipokwisha msifu*
*Sultani maarufu*
*Na ashrat aalafu*
*Dinari kamuatia*

*Takupa watu wengine*
*Maidani mpigane*
*Niwe papa nikuone*
*Name hikushuhudia*

*Nawatimie elfu*
*Mashujaa waso khofu*
*Wawezao kita sefu*
*Wazoevu wa kitaa*

Waliweka mkataba wao na ulipokamilika, vita vilianza. Mikidadi alipigana na askari wale lakini akaamua kutowaua na badala yake akawatia alama wote, na kumpa Sultani ripoti ile. Sultani aliamrisha kuwa askari wale wote wauawe, na basi Mikidadi akawa hana budi ila kurudi vitani na kuwaua mashujaa wote akiwemo shujaa wao wa mji. Sultani kuona vile, alimwita waziri na kumwambia ampe Mikidadi kila kitu alichokihitaji.

Kupigana huku kwa Mikidadi kunadhihirisha ujasiri unaomfanya Mikidadi mtu wa kiajabu sana. Mikidadi alipigana na askari elfu moja ambao wamefunzwa kupigana naye Mikidadi hajafunzwa kupigana. Kupigana huku kusikokuwa kwa kihalisia ndiko kunakochochea mtafiti kuunasibisha na tukio la kihalisiamazingaombwe.

***Kupigana kwa Mikidadi na Simba wa Sultani***

Mikidadi alipopewa mali aliyohitaji na Sultani alianza safari kuelekea kwa Khamisi. Alipofika huko, alielezwa kuwa, huko nyuma, mali yote ilikuwa imechukuliwa na kundi fulani la watu. Mikidadi alilifuata kundi lile na kuua watu wengi, na akachukua silaha zao na mali yote. Waziri akamuendea Sultani kumueleza yaliyotokea, lakini akawa ana wazo ambalo alidhani akimshauri Sultani alikubali, wangemumaliza Mikidadi. Waziri alimshauri Sultani ampe Mikidadi simba wake apigane naye ili aweze kumwangamiza Mikidadi. Simba huyo alikuwa akipambwa kwa dhahabu na lulu na alikuwa akimla binadamu mmoja kila siku kama inavyoelezewa katika ubeti wa 450:

*Simba huyu hali kitu*
*Hali manyama ya mwitu*
*Kila siku hula watu*
*Sultani kamwambia*

Sultani alikubali, lakini badala ya simba ambaye alikuwa amezoea kuwala watu, kumwangamiza Mikidadi, Mikidadi ndiye aliyemwangamiza simba yule. Haya yanazungumziwa katika ubeti wa 456:

*Alipokwisha mkata*
*Simba akamkukuta*
*Na shairi akaleta*
*Kijisifu ushujaa*

Kabira (1998) ananazungumzia hali ya mashujaa kuwa na nguvu za kiajabu kama hizi Mikidadi kuweza kupigana na kumshinda samba. Anasema, 'baadhi ya sifa ambazo mashujaa katika tendi hudhihirisha ni kama: weledi kwa vita, maumbile ya kiajabu na nguvu za kupita kiasi' (tafsiri yetu) (Kabira, 1998). Vita hivi vya Mikidadi na simba wa Sultani ni tukio la uhalisiamazingaombwe, kwani kihalisia binadamu si rahisi apigane na simba na kumuua hivihivi, bila kujiandaa vilivyo.

***Kupigana kwa Mikidadi na Jeshi la Malik***

Shujaa Mikidadi aliporudi na mahari ili amuoe Mayasa alisikia kwamba kulikuwa na harusi kati ya Mayasa na Malik iliyokuwa ikiendelea. Mayasa alikuwa amezingirwa na askari wengi ambao walikuwa wanamsindikiza kwa mume wake mtarajiwa, Malik. Kulingana na Jabbar (2004), shujaa huwa na sifa zinazokiuka kaida za maumbile. Mikidadi alipogundua kuwa Mayasa ndiye aliyekuwa akipelekwa kwa Malik, alipiga kelele kama radi kusudi kuwaogofya na kuwaonya wahusika wamwachilie Mayasa. Aliwaamrisha waangushe silaha zao, ikiwa waliyathamini maisha yao. Katika ubeti wa 542 anasema:

*Muateni mwende vyenu*
*Muokoe roho zenu*
*Huyuno si mke wenu*
*Siye mke wa kuoa.*

Askari walighairi, na vita vikaanza. Mikidadi aliwakatakata vichwa. Ubeti wa 557 unaelezea haya:

*kati kawangia mwao*
*asikhofu wingi wao*
*kiwakata vitwa vyao*
*asipumue kuua*

Wanajeshi wengine walipoona jinsi Mikidadi alivyokuwa akiwaangamiza wenzao, walimwachilia Mayasa, na Mikidadi akamwendea. Mayasa alimwambia Mikidadi apigane na jeshi hilo, atwae mali yao, kisha warudi kwao bila kitu. Kwa hasira, Mikidadi alimwambia Mayasa kuwa atalimaliza jeshi hilo lote, na wahusika hawatarudi makwao. Katika ubeti wa 554 anasema:

*Akajibu Mikidadi*
*Hawa kwao hawarudi*
*Roho zao na jasadi*
*Haibudi kupotea*

Mikidadi alipigana na kuwaua wengi wao. Waliobaki ni wale waliokimbia na kuacha mali na silaha zao. Tukio la Mikidadi kuwaangamiza watu wengi ni la kiajabu kwa sababu hili ni jeshi ambalo limefunzwa jinsi ya kupigana ilhali Mikidadi ni mtu wa kawaida tu. Japo shujaa hukumbana na pingamizi kubwa katika kutekeleza majukumu yake kama anavyodokeza Meyer (1993), pingamizi ya askari waliokuwa wamemzingira Mayasa haikumzuia Mikidadi kumpata Mayasa. Alipigana vita vya kiajabu hadi akampata Mayasa.

***Kupigana kwa Mikidadi na Simba wa Mungu***

Shujaa huwa na sifa za kiajabu na nguvu za kiungu (Hale na Belcher 1997). Sifa anazopewa Mikidadi ndizo zinazomwezesha kupigana na watu wengi na kuwashinda. Mikidadi na Mayasa walipokuwa wakienda kwao, waliona farasi wawili katika kundi lililokuwa linapita. Mayasa alipotazama vizuri, aliona taji zuri lililokuwa limevaliwa na akalitamani. Kwa vile Mikidadi alitaka Mayasa apate kila kitu alichokihitaji, alienda kundini na kuomba lile taji. Ali mwenye taji alikataa kumpa, na basi Mikidadi wakaanza kupigana na Ali. Walipigana usiku kucha. Waliendelea tena hadi alasiri. Wakiwa vitani, Ali alimwambia Mikidadi kuwa yeye ni Simba wa Mungu (Ali) na basi hakuna mchezo pale! Wawili hawa walipigana sana hadi Mikidadi akaona kuwa ameshindwa hakika. Anaporejea kwa Mayasa, Mayasa anamwambia kuwa anaona kana kwamba hataki kumletea lile taji. Haya yamo katika ubeti wa 606:

*Kawana mara ya pili*
*Kapotewa na akili*
*Akarudi tashili*
*Kwa Mayasa kurejea*

Mayasa anamwambia kuwa asipomletea lile taji basi ataenda kupigana ili alitwae. Mikidadi aliposikia maneno ya Mayasa alirudi kupigana tena na mwishowe alishindwa vita na Ali. Mikidadi anaposhindwa vita na Ali, Mayasa ndiye anayekuwa wa kwanza kumtetea kwa Ali ili asimwangamize. Katika ubeti wa 621:

*Simuue Haidari*
*Zidi moyo kusubiri*
*Akatoa na shairi*
*La kumsifu Alia*

Mayasa anamkariria Ali shairi ambalo linamsihi asimwangamize Mikidadi. Kutokana na jinsi alivyopigana kwa ujasiri, Ali aliamua kumsilimisha Mikidadi. Mikidadi na Mayasa basi wakasilimishwa! Haya yanazungumziwa katika ubeti wa 632 na ubeti wa 636:

*Naye mkewe Mayasa*
*Akisa akafuasa*
*Kashahadia kabisa*
*Na Mikidadi pamoja*

*Mikono yako inua*
*Uisome hino dua*
*Rabi takupa afua*
*Shida ya dunia*

Tukio la uhalisiamazingaombwe ni kule kupigana kwa Mikidadi na Ali kwa muda mrefu, licha ya kwamba Ali ni Simba wa Mungu. Binadamu wa kawaida hawezi kupigana na Mungu au malaika wake kwa sababu Mungu ndiye aliyeumba binadamu, na pia ana uwezo mwingi kumshinda. Ali angempiga mara moja na amwangamize Mikidadi kwa vile Mikidadi ni binadamu wa kawaida ilhali Ali ana nguvu za kiungu. Licha ya nguvu hizo za kiungu, Mikidadi alistahimili vita kwa takriban siku moja na nusu. Huu ni uhalisiamazingaombwe kwani kama inavyodaiwa na mhimili wa pili, uhalisiamazingaombwe huweza kuvunja mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa. Katika kupigana huku, mpaka wa kimataifa umevunjwa kwa sababu katika hali ya kawaida haiwezekani kupigana na kiumbe wa Mungu.

## Hitimisho

Makala hii imeangazia uhalisiajabu katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Waandishi waliongozwa na mihimili miwili ya Nadharia ya uhalisiamazingaombwe katika kutambulisha matukio ya uhalisiamazingaombwe kupitia kupigana kwa mhusika Mikidadi. Wa kwanza ikiwa kuwa matukio ya kiajabu huonekana ya kawaida na pia ya kuogofya. Kupitia mhimili wa pili waandishi waliweza kuonyesha kuvunjwa kwa mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa kutoka na matukio hayo ya Mikidadi ya kihalisiamazingaombwe. Makala hii inadhihirisha kuwa Mikidadi, japo amechorwa kama kiumbe wa kawaida, ni mhusika wa kihalisiamazingaombwe. Haya yanathibitishwa kupitia vita kati yake na wahusika mbalimbali katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Mikidadi ameweza kupigana na wahusika hao katika namna isiyo ya kawaida na akawashinda bila tashwishi yoyote. Ni mhusika mmoja tu aliyeweza kumlemea Mikidadi kwa sababu ya uungu wake, hali ambayo inaeleweka. Kwa kuhitimisha, Makala hii inadhihirisha kuwa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* una matukio ya kihalisiamazingaombwe kupitia kupigana kwa mhusika Mikidadi.

## Marejeleo

Alexander, M. (1990) *Flights from realism*. London. Edward Arnold.

Danow, D. (1995) *The spirit of carnival:Magical realism and the grotesque*. Kentucky: The University press of Kentucky.

Elbuhry, A. (1932). *Utendi wa mikidadi na Mayasa(10th ed.)*. Oxford. Azania Press.

Halle, A. na Belcher, S. (1997) *Oral literature from Africa*. Vibrant Voices from Vast Continent. Indiana University Press.

Jabbar, L. (2004*) Concept of heroism Beowulf and Gawain and the green knight*. (M.A) Baghdad.

Kabira, M. (1998) *Oral LITERATURE*. College of Education and External Studies. University of Nairobi Press.

Meyer, A. (1993) *A glossary of literary terms*. Epics and Epic Heroes

Microsoft publisher Limited (2000) In Encarta. New York.

Nyambung'a, V. (2005) *Uhakiki wa bina-adamu*! (2002) na *Musaleo!* (2004). (M.A) Nairobi.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Rogers, H. (2002) *Word Work: surviving and thriving as a writer*. Invisible Cities Press.

Roh, F. (1925) *Narch-expressionismus-magischer realismus*. *Probleme der neueste europaischen Malerei*. Leipzig: Klinkhardt & Biermann.

Walibora, K. (2010) *Uhalisia na uhalisiamazingaombwe*: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum Swahili Forum (17), 143.

Wamitila, K. (2008) *Kanzi ya fasihi*. *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

Warnes, C. (2006) Magic realism and the legacy of german idealism. *The Modern Language Review*, 101(2), 488.

Zamora, P. (1995) *Magic realism*. Dhurham. Duke University Press.